



Sikukuu ya Pasaka



Tusome Early Literacy Programme

Sikukuu ya Pasaka




Familia ya Bukeko ina watoto wanne.

Wasichana wawili na wavulana wawili.

Wakati wa sikukuu ya Pasaka, waliamua kwenda
mjini kununua mavazi.

Wote walipanda gari lao na kuelekea mjini.






Walipofika mjini, Bukeko aliingia kwenye benki
kutoa pesa.

Ndani ya benki, alimkuta meneja aliyevalia buibui.

Meneja alimuelekeza kwa karani wa benki aliyevalia suti ya samawati.

Karani wa benki alimpattia Bukeko shilingi elfu ishirini na tano.





Bukeko alirudi kwenye gari lake akiwa na furaha tele.
Alimpatia kila mtoto shilingi elfu tano za kununua
mavazi.

Walielekea kwenye duka moja la mavazi.

Walimkuta mlinzi aliyevalia sare ya manjano.





Mlinzi aliwaelekeza ndani kwa mwenye duka.
Mwenye duka aliwaonyesha mavazi mbalimbali.

Wavulana walinunua kaptura nyeusi, mashati ya samawati na makoti meupe.

Baada ya kulipa, walibakisha shilingi elfu moja kila mmoja.






Wasichana walinunua blauzi nyekundu, sketi za manjano na leso nyeupe.

Pia, walinunua suruali nyeusi na fulana za samawati.

Baada ya kulipa, wasichana hawakubaki na pesa zozote.

Walimuomba baba yao Bukeko awaongezee pesa ili wanunue viatu vyeupe.





Baba yao aliwaomba wavulana wawasaidie dada zao.

Wavulana waliwapatia dada zao shilingi elfu moja.



Wasichana walifurahi sana.

Waliahidi kuwanunulia kaka zao kofia wakati wa sherehe za kuzaliwa kwao.

Maswali

1. Familia ya Bukeko ina watoto wangapi?
2. Kwa nini familia ya Bukeko iliamua kwenda mjini?
3. Mlinzi alivalia sare ya rangi gani?
4. Wavulana walinunua nini?
5. Wasichana waliahidi kuwanunulia nini kaka zao?

Sikukuu ya Pasaka

Ni wakati wa sikukuu ya Pasaka.
Familia ya Bukeko inaenda mjini
kununua mavazi mbalimbali. Je,
watanunua mavazi ya aina gani?



Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka
kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la
Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo
ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kuitia
mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.